hamani ya samaki waliozalishwa mwaka 2021 Ziwa Tanganyika

# Kampeni ya usimamizi uvuvi ziwa Tanganyika yashika kasi

**Na MWANDISHI WETU**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amezindua kampeni ya kitaifa ya uelewa kuhusu mkataba wa kikanda wa usimamizi wa uvuvi endelevu wa Ziwa Tanganyika.

Mpango huo ni miongoni mwa sehemu ya serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuja na mikakati mbalimbali ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika ziwa hilo.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa uzinduzi wa mkataba huo uliofanyika mwalo wa Kabwe, mkoani Rukwa, Waziri Ndaki

alisema kampeni hiyo ni miongoni mwa hatua za utekelezaji wa mkataba unaojumuisha nchi zinazonufaika na uvuvi wa Ziwa Tanganyika.

Alizitaja nchi hizo kuwa ni Tanzania, Burundi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo

"Sote tunafahamu samaki hawana mipaka na huwezi kuwapangia maeneo ya kwenda ndani ya ziwa, hivyo tukaona ni vema tukawa na mwongozo wa pamoja baina ya nchi hizi zinazohusika na Ziwa Tanganyika ili tuwe na lugha moja katika utekelezaji wa kanuni na utaratibu unaopaswa kufuatwa kwa wavuvi waliopo nchi husika," alisema.

Waziri Ndaki aliwaagiza watalaamu wa sekta ya uvuvi waliopatiwa semina elekezi kuhusu mkataba huo, kuhakikisha wanafikisha elimu kwa wavuvi ambao ndiyo walengwa wa mkataba huo ili wauelewe kabla ya kuanza kuutekeleza.

"Mkaitishe mikutano ya wavuvi moja kwa moja mkawaelimishe, msiishie kwa viongozi wa kata au serikali za vijiji kwa sababu mara nyingine hao hawaendi ziwani na hata changamoto za wavuvi hawazijui," aliagiza.

Aidha, alitoa rai kwa wananchi wanaojihusisha na uvuvi Ziwa Tanganyika kuwa tayari kujitokeza kwa wingi kupata elimu watakapohitajika kuhusu mkataba huo, ili watoe maoni yenye lengo la kuuboresha kabla ya kuanza kutekelezwa.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mwanamvua Mrindoko,

ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Katavi, alitaja miongoni mwa changamoto zilizokuwa zikiikabili sekta ya uvuvi katika mikoa inayopitiwa na Ziwa Tanganyika ni utoroshwaji wa rasilimali za uvuvi kwenda nje ya nchi kupitia maeneo ya mipakani.

Nyingine ni baadhi ya wavuvi kuvamiwa na kuporwa mali zao, hivyo ana amini mkataba huo utaondoa changamoto hizo.

Akizungumzia kiwango cha samaki wanaovuliwa katika ziwa hilo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia Sekta ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema Ziwa Tanganyika huchangia takribani asilimia 19 ya samaki wanaozalishwa nchini.

Aliongeza kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2021, ziwa hilo lilizalisha tani 90,743 zenye thamani ya sh. bilioni 592.5.

Naye, Mkurugenzi wa Kanda wa Uvuvi na Ufugaji wa Samaki, Mamlaka ya Ziwa Tanganyika, Beatrice Marwa, alibainisha uvuaji wa samaki wachanga katika ziwa hilo kwa upande wa Tanzania unasababisha upotevu wa zaidi ya dola za Marekani 690,000 kila mwaka huku nchi ya Zambia ikipoteza zaidi ya dola za Marekani milioni moja kutokana na kitendo hicho.

Uzinduzi wa kampeni hiyo hapa nchini ulifanyika baada ya nchi za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Zambia na Burundi kufanya hivyo takribani wiki mbili zilizopita, lengo likiwa ni kuunganisha nguvu ya pamoja katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi wa Ziwa Tanganyika na kuufanya kuwa endelevu.

## UZINDUZI



**WAZIRI** wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (katikati), akikata utepe kuzindua kampeni ya kitaifa ya uelewa kuhusu Mkataba wa Kikanda wa Usimamizi wa Uvuvi Endelevu katika Ziwa Tanganyika, kwenye Mwalo wa Kabwe,Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, mwishoni mwa wiki. Kutoka kushoto ni Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mwanamvua Mrindoko, Katibu Mkuu wa wizara hiyo (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah na Mkurugenzi wa Uvuvi na Ufugaji wa Samaki wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika, Beatrice Marwa. (Na Mpigapicha Wetu).

UHURU UK 15.

## ayofanywa mkoani Songwe

# we
# ingo

nga mazoea ya
apotoa huduma
moja na wateja
kuhudumiwa, ili
TRA na serikali
kufanya hivyo
di za serikali

Meneja wa TRA
Dickson Kimaro,
sa wa mamlaka
makuu, utasaidia
aji mapato na
za walipakodi

u wa TRA Makao
Mwakasendile,
ngo kwa Mlango
a walipakodi ili
a kuwaelimisha
gea utayari.



# ufuga

a husika ili

uamuzi
o ni mzuri,
utapunguza
maadili kwa

wa mamlaka
huo msaada
ri na vijana

aidia kwani,
uhalifu na
a wanafanya

aji...

# Wizara ya Mifugo yaibuka kidedea tuzo Utawala Bora

**Na MWANDISHI WETU**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), imeshika nafasi ya pili katika tuzo za Utawala Bora zinazotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kutokana na utoaji wa huduma bora kwa watumishi na wananchi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Akipokea tuzo hiyo jijini Dodoma jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Tixon Nzunda, alisema tuzo hiyo, imepatikana kutokana na ushirikiano mkubwa na kufanya kazi kama timu, weledi, uadilifu na uwajibikaji kwa umma.

"Nitumie fursa hii, kuwashukuru watumishi wote wa wizara ya mifugo na uvuvi kwa kuwezesha tuzo hii kupatikana, tumefanyiwa tathimini katika eneo la

> **Nitumie fursa hii, kuwashukuru watumishi wote wa wizara ya mifugo na uvuvi kwa kuwezesha tuzo hii kupatikana...**
>
> Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Tixon Nzunda.

utawala bora ambapo tumeshika nafasi ya pili, tuchukue hii kama changamoto kwa kufanya vizuri zaidi.

"Nishani hii ni kama chachu ya kufanya mabadiliko makubwa ili mwaka ujao tusiongoze tu katika masuala ya utawala bora, ushughulikiaji wa malalamiko, taarifa za watumish.

"Pia, tuwe vinara katika kusimamia miradi ya maendeleo ya sekta zetu, kuanzia minada, mabwawa, visima, majosho, ufuatiliaji wa miradi na kuhakikisha kwamba, thamani ya fedha ya miradi yetu inapatikana," aliongeza

Awali, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Sekta ya Mifugo, Dk. Charles Mhina, alisema tuzo hiyo ya utendaji bora, imetolewa Mei 27, mwaka huu kwa wizara hiyo (Sekta ya Mifugo) kwa kufanya vizuri katika uingizwaji wa taarifa sahihi katika mfumo wa taarifa za utumishi.

Vigezo vingine ni uhuishaji taarifa kwenye mfumo kwa wakati, ushughulikiaji wa malalamiko ya watumishi na wananchi kwa wakati, kuzingatia na kutekeleza sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na sheria mbalimbali za nchi katika kazi zote za kila siku.

Tuzo hizo zinazotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kila mwaka, zinajumuisha wizara zote zilizopo Tanzania bara.

Nfasi ya kwanza imetwaliwa na Ofisi ya Rais Ikulu, nafasi ya pili imechukuliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na nafasi ya tatu, imekwenda kwa Wizara ya Fedha na Mipango.

CamScanner

KIKAO>>Kazi cha uchamb

* UHURU UK 8 *

# DC Kilosa awaonya wafugaji wanaochapa viboko wakulima

**Na LATIFA GANZEL,** *Morogoro*

SERIKALI wilayani Kilosa, mkoani hapa, imewataka wafugaji kuacha mara moja tabia ya kujichukulia sheria mkononi na kufanya fujo katika mashamba ya wakulima kwa kuwachapa viboko.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga, alisema hayo jana, wakati wa hafla fupi ya kukabidhi mbegu 16 za ng'ombe na saba za mbuzi kwa wafugaji wa Kijiji cha Mbwade, Kata ya Madoto.

Ng'ombe na mbuzi hao, waliotolewa na Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT) kupitia mradi wa kuleta ushirikiano kati ya wakulima na wafugaji (FPC).

Aliwataka kuungana pamoja kutokomeza migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa kero katika wilaya hiyo.

"Baadhi ya wafugaji wilayani humu wamekuwa na tabia ya kuwachapa viboko wakulima, hali inayosababisha kujenga uhasama baina ya jamii hizo mbili," alisema.

Aliwaagiza viongozi wa kimila wa jamii ya kimasai kukomesha tabia hiyo kwa kukutana na kuzungumza.

Mkurugenzi wa SAT, Janeth Maro, alieleza kupitia mradi wa FPC wanawajengea uwezo wakulima na wafugaji kufanya kilimo endelevu na ufugaji bora, lengo likiwa ni kuondokana na migogoro baina yao.

Kuhusu ugawaji wa mbegu za ng'ombe na mbuzi kwa wafugaji, Janeth alibainisha umeenda na utoaji elimu ili wafugaji wafuge na kuzalisha mifugo mingi yenye tija itakayowasaidia kuongeza kipato chao na cha taifa kwa ujumla.

> **Baadhi ya wafugaji wilayani humu wamekuwa na tabia ya kuwachapa viboko wakulima, hali inayosababisha kujenga uhasama baina ya jamii hizo mbili...**
>
> Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga

Alisema zaidi ya ekari 1,000 zimetengwa kwa malisho yatakayowasaidia wafugaji kulisha mifugo yao, wakati wa kiangazi ili isife kwa kukosa chakula kwa kipindi kirefu.

Alifafanua kwamba mashamba hayo yameanzishwa kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, ambayo kwa sasa yanaathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za kilimo na ufugaji hususan kwa wanaozifanya kwa mazoea.

Mwakilishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sebastian Shilangalila, alipongeza SAT kwa kazi inayofanya ya kuelimisha wafugaji kufuga kisasa na kuondokana na migogoro baina yao na wakulima.

Mwenyekiti wa wafugaji, Wilaya ya Kilosa, Mkunwa Suhani, alisema ujio wa mbegu hizo utaleta mageuzi makubwa kwa wafugaji kwa kuwa awali walikuwa wakifuga kienyeji, hali iliyosababisha kuwa na mifugo mingi isiyo na tija na migogoro.

Dk.
ma

WA



MKUU
Chuo
(Picha

Se

Na ASI

SERIKA
cha B
miund
kufund
Kau
Salaam
Uchuk
akifun
wa bu
Ko
la kwa
wa bu
zinazo
taifa.
Ali
Posta,
inaang
kubwa
chuo k
Mw
imete
mfum
"N
karibu
miun